

Narumbe 5/2/63

Wakoloni wako mavini - Moshi

MANENO ya mwaka 1959 ya Mwalimu Julius Nyerere kwamba Watanganyika watawasha kileleni Kilimanjaro mwangaza wa matumaini kwa watu wa nchi za jirani zenye chuki, yametamkwa kwa mara nyingine na Waziri wa Mambo ya ya Ndani ya Nchi Bwana Kambona.

Akiufungua m' u'aro wa Umoja wa Nchi za Afrika na Asia huko Moshi jana kuwakaribisha wajumbe kwenye mkutano huo alisema; kusudi la Rais Nyerere la mwaka 1959, limethibitishwa na mkutano huu uliofunguliwa kando kando ya mlima Kilimanjaro mbele ya wajumbe hao.

Bwana Kambona badaye alichaguliwa mwenye kiti wa mkutano huo. Akigusia juu ya uhuru wa Afrika kwa jumla, alisema, baada

ya Tanganyika kujitawala, ilifuatia Uganda na Burundi, hii leo Malawi nayo imejipatia madaraka ya ndani. Kina Kauda nao wamo njiani kuelekea kulivunja shirikisho la Wakoloni wakiwa mbioni kuelekea kujitawala.

Kulikuwa hakuna shaka yeyote kwamba Afrika Kusisi nayo itaokoka katika muda si mrefu. Hatua hii itakapofikiwa aliendelea, ndugu zetu huko watakuwa tayari kutufikia bila wasiwasi.

Wale roho mbaya

Kulikuwa na masha msham makubwa kutokea kwa mijitu yenye roho mbaya kwamba mkutano huu utashindwa kufaulu. Lakini ni lazima watambue kuwa ku ngali na sehemu nyingi ulimwenguni ambazo bado zinatawaliwa, ni wazi kwamba mkutano wa aina hiyo, sio upotezaji wa wakati. Nafasi hiyo ya kifungu cha maneno il pigiwa makofi sana na mkutano huo. Anasema mwandishi wetu Moshi.

Bwana Kambona ali maliza hotuba yake kwa kuutakia heri mkutano huo, na akauomba uake macho sana hasa katika kuzungumza ni hatua gani zichukuliwe ku maliza ukoloni katika sehemu za Afrika zinazotawaliwa bado.